



ACTION2DAY PRESS

St. Nicholas

The saint who gave in secret

English · Kiswahili



Long ago, in a town called Patara, a baby named Nicholas was born. His parents loved God and had great wealth.

Zamani sana, katika mji wa Patara, alizaliwa mtoto aitwaye Nicholas. Wazazi wake walikuwa Wakristo matajiri waliompanda Mungu sana.



Nicholas grew up hearing stories of Jesus. He learned to love God and to care for others, especially the poor.

Nicholas alikua akisikiliza hadithi kuhusu Yesu. Alijifunza kumpenda Mungu na kuwajali wengine, hasa masikini.



When Nicholas was still young, both of his parents got very sick and died. They left him a large amount of money.

Nicholas alipokuwa bado mdogo, wazazi wake walipatwa na ugonjwa na wakafariki dunia. Walimuachia mali nyingi.



Nicholas heard of a poor man with three daughters who had no money for getting them out of slavery. One night, he secretly dropped a bag of gold into their home.

Nicholas alisikia kuhusu baba maskini mwenye mabinti watatu. Usiku mmoja, akatupa mfuko wa dhahabu dirishani mwao bila kujulikana.



The father caught Nicholas giving again. He thanked Nicholas, but Nicholas asked him to thank God instead.

Baba alijificha usiku na akamwona Nicholas akitoa zawadi tena. Alimshukuru Nicholas, lakini Nicholas alimtaka amshukuru Mungu.



Nicholas wanted to serve God even more. He traveled to a city called Myra, trusting God to lead him.

*Nicholas alitaka kumtumikia Mungu zaidi.
Akasafiri hadi mji wa Myra, akimtegemea Mungu
amwongoze.*



The church leaders in Myra were praying for a new bishop. They believed God had chosen Nicholas, and they made him their bishop.

Viongozi wa kanisa walikuwa wakimuomba Mungu awape askofu mpya. Wakaamini Mungu alimchagua Nicholas, na wakamteua kuwa askofu wao.



When a famine came, the people were starving. Nicholas prayed, and soon, ships full of grain arrived in the harbor.

*Njaa ilipotokea, watu waliteseka sana.
Nicholas aliomba kwa Mungu — kisha meli
zilizojaa nafaka zikatua bandarini.*



On a ship journey, a terrible storm hit. Nicholas prayed, and the wild winds stopped. The sailors were saved.

Wakiwa safarini baharini, dhoruba kali iliwakumba. Nicholas akaomba kwa Mungu, na upepo mkali ukatulia. Wasafiri wakaokoka.



Three innocent men were about to be punished for a crime they didn't do. Nicholas rushed in just in time to stop it and told the truth.

Wanaume watatu walikuwa karibu kuuawa kimakosa. Nicholas aliwasili kwa haraka, akasimulia ukweli, na akawaokoa.



An evil butcher harmed three boys. Nicholas found them and prayed.

Muza nyama mwovu aliwadhuru watoto watatu. Nicholas aliwapata, akaomba kwa Mungu.



And by a miracle, they came back to life.

Na kwa muujiza, wakafufuka!



Nicholas helped build a beautiful church where people could worship Jesus and learn about God's love.

Nicholas alisaidia kujenga kanisa zuri lililoitwa kwa jina la Yesu, ambako watu walimwabudu Mungu kwa furaha.



Many people who were sick came to Nicholas. He prayed for them, and God healed their bodies and gave them hope.

Wagonjwa wengi walimjia Nicholas. Aliwaombea, na Mungu akawaponya na kuwapa tumaini.



At night, Nicholas would leave sweet treats, coins, and little gifts in the shoes or socks of poor children.

Usiku, Nicholas aliziweka kwa siri zawadi ndogo, pipi au sarafu, kwenye viatu au soksi za watoto maskini.



A wicked emperor did not like Christians. Nicholas was arrested and thrown into jail for his faith.

Mfalme mwovu hakuwapenda Wakristo. Nicholas alikamatwa na kufungwa gereza kwa sababu ya imani yake.



Years later, Emperor Constantine ended the persecution. Nicholas was set free and returned home to serve again.

Miaka baadaye, Mfalme Constantine alikomesha mateso kwa Wakristo. Nicholas aliachiliwa na kurudi nyumbani.



At a big church meeting called the Council of Nicaea, Nicholas boldly defended the truth about Jesus Christ.

Katika mkutano mkubwa wa kanisa uitwao Baraza la Nicaea, Nicholas alitetea ukweli kuhusu Yesu kwa ujasiri.



Nicholas taught everyone — rich or poor — to be kind, to forgive, and to love like Jesus.

Nicholas aliwafundisha watu wote — maskini na matajiri — kupenda, kusamehe, na kuishi kama Yesu.



Even when Nicholas was old, he never stopped caring for people. He gave, prayed, and helped every day.

Hata alipozeeka, Nicholas hakuacha kuwasaidia watu. Alitoa, aliomba, na alipenda bila kuchoka.



On December 6, Nicholas passed away. People were sad — but they remembered his loving heart.

Tarehe 6 Desemba, Nicholas alifariki kwa amani. Watu walihuzunika lakini wakamkumbuka kwa moyo wake mwema.



Everywhere people told the story of Bishop Nicholas — the man who gave in secret and loved deeply.

Nicholas became known as Saint Nicholas. Many churches were named after him, and his story spread far and wide.

Kila mahali, watu walieleza hadithi ya Askofu Nicholas — mtu aliyejawa na upendo wa Mungu na roho ya kutoa.

Nicholas akawa maarufu kama Mtakatifu Nicholas. Majumba ya ibada mengi yakawekwa kwa jina lake duniani kote.



Because of his generous heart, people began giving gifts in December to remember Saint Nicholas.

Watu walianza kutoa zawadi Desemba wakimkumbuka Nicholas kwa ukarimu wake.



Over the years, Saint Nicholas' story became part of Christmas joy — and inspired the jolly Santa Claus we know today!

Miaka ilivyopita, hadithi ya Mtakatifu Nicholas ikawa sehemu ya furaha ya Krismasi — na ikamhimiza kuibuka kwa Santa Claus mchangamfu tunayemfahamu leo!



Painted & edited by

Action2day Art Center · Nairobi

Fabian Romain Lashley
Griffins Nyangaresi Museti
Steve Mugiraneza Rukeramihigo
Caleb Gathii Manyera
Abigael Nyaboke Nyakundi
John Maina Onyango

Irene Kiviya Nduku
Ecclesiastes Madaraka Medo
Kristian Juma Omedo
Maxwell Mukanga Indukule
Angel Miriam Mlenda